

WAZIRI Mkuu Mstaafu wa Tanzania, Mhe. Mizengo amesema kuwa amefurahishwa na bidhaa zilizopo ndani ya banda hilo pamoja na elimu inayotolewa kwa wananchi kuhusu kilimo, mifugo, uvuvi na ujasiriamali.



Kauli hiyo ameitoa, Agosti 01/2023 wakati alipotembelea banda la Halmashauri ya Manispaa Morogoro katika maonesho ya Nane Nane yanayofanyika kwenye uwanja wa Julius Kambarage Nyerere, Morogoro.



Kwa upande mwingine, Mheshimiwa Pinda, amempungeza Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mstahiki Meya Manispaa ya Morogoro, Baraza la Madiwani, Mkurugenzi wa Manispaa pamoja na viongozi wote waliofanikisha maandalizi ya banda hilo huku akionesha kuvutiwa zaidi na kilimo cha Mjini.



Hata hivyo, amesema kuwa ili uchumi wa nchi ukue, tunategemea viwanda na malighafi ambazo nydingi tunazipata mashambani, hivyo kwa Kanda ya Mashariki inayohusisha Mikoa ya Tanga, Pwani Dar es salaam na Morogoro ina uwezo mkubwa wa kuzalisha chakula kwa kasi na kufikia azma ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kulisha Bara la Afrika kutokana na Kilimo chenye tija.



Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, ndugu Ally Machela, ametoa wito kwa wananchi pamoja na wakulima kufika katika banda la Manispaa ili kujionea bidhaa bora na kupata elimu ambayo itakuwa na tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji.

Maonesho ya NaneNane yameanza Agosti 1 yatamalizika Agosti 8, 2023 nchi nzima ambapo kauli mbiu ya mwaka huu 2023 ni "Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula".

MWISHO